# Biblia kwa wana

zawadi

# Kuzaliwa kwa Yesu



Iandiligwe na: Edward Hughes

Imeonyeshwa na: M. Maillot
Alastair Paterson

Imebadilishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.

Ilitafsiriwa na: www.christian-translation.com

Iliyotengenezwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2021 Bible for Children, Inc.
Leseni: Una haki ya kunakili au kuchapisha hadithi hii, mradi hauiuzi.



Zamani sana, Mungu alimtuma malaika Gabrieli kwa msichana mzuri wa Kiyahudi aliyeitwa Mariamu. Akamwambia, "Utapata mtoto wa kiume na kumwita jina lake Yesu. Yeye ataitwa Mwana wa Aliye juu. Atatawala milele."




"Je! Hii inawezaje?" msichana huyo alishangaa aliuliza. "Sijawahi kuwa na mwanaume yeyote." Malaika alimwambia Mariamu mtoto atatoka kwa Mungu. Hakutakuwa na baba wa kibinadamu.
3


Kisha malaika akamwambia Mariamu kwamba binamu yake Elizabeth alikuwa na mtoto katika uzee wake. Huu pia ulikuwa muujiza. Muda mfupi baadaye, Mariamu alimtembelea Elizabeth. Walimsifu Mungu pamoja.
4


Mariamu alikuwa ameolewa na mwanamume anayeitwa Yusufu. Yusufu alihuzunika aliposikia Mariamu alikuwa anatarajia mtoto. Alidhani mtu mwingine ni baba.
5


Katika ndoto, malaika wa Mlungu alimwambia Yusufu kwamba mtoto huyu alikuwa Mwana wa Mungu. Yusufu alikuwa amsaidie Mariamu kumtunza Yesu.
6


Yusufu alimwamini na kumtii Mlungu. Pia alitii sheria za nchi yake. Kwa sababu ya sheria mpya, yeye na Mariamu waliondoka kwenda mji wao, Bethlehemu, kulipa ushuru.
7


Mariamu alikuwa tayari kupata mtoto wake. Lakini Yusufu hakuweza kupata chumba mahali popote. Nyumba zote za wageni zilikuwa zimejaa.
8


Hatimaye Joseph alipata zizi. Hapo, Mtoto Yesu alizaliwa. Mama yake alimlaza kwenye hori la ng'ombe, mahali ambapo chakula cha wanyama kilikuwa kikiwekwa kawaida.
9


Karibu, wachungaji walinda mifugo yao iliyokuwa imelala. Malaika wa Mlungu alitokea na kuwaambia habari hizo za ajabu. "Leo amezaliwa katika mji wa Daudi Mwokozi Ambaye ndiye Kristo Bwana. Utakuta Mtoto amelazwa horini."
10


Ghafla, malaika wengi zaidi mkali walitokea, wakimsifu Mlungu na kusema, "Utukufu kwa Mungu aliye juu na duniani amani, mapenzi mema kwa wanadamu."
11


Wachungaji walienda haraka kwenye zizi. Baada ya kumuona Mtoto huyo waliwaambia kila mtu walikutana na yale ambayo malaika walikuwa wamesema juu ya Yesu.
12


Baadaye, Yusufu na Mariamu walimleta Yesu kwenye hekalu huko Yerusalemu. Hapo mtu mmoja aliyeitwa Simeoni alimsifu Mlungu kwa Mtoto, wakati mzee Anna, mtumishi mwingine wa Bwana, alishukuru.
13


Wote wawili walijua Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, Mwokozi aliyeahidiwa. Yusufu alitoa dhabihu kwa ndege wawili. Hii ndiyo sadaka ya sheria ya Mlungu iliyosema watu masikini wanapaswa kuleta wakati wanapomletea Bwana mtoto mchanga.
14


Wakati fulani baadaye, nyota maalum iliwaongoza Wenye Hekima kutoka nchi
ya Mashariki kwenda Yerusalemu. "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" waliuliza. "Tunataka kumwabudu."
15


Mfalme Herode alisikia kuhusu Wajanja. Akiwa na shida, aliwauliza wamwambie wanapompata Yesu. "Ninataka kumwabudu Yeye pia," Herode alisema. Lakini alikuwa akisema uwongo. Herode alitaka kumwua Yesu.
16


Nyota iliwaongoza Wenye Hekima kwa nyumba ileile ambayo Mariamu na Yusufu waliishi na Mtoto mchanga. Wakipiga magoti katika ibada, wasafiri hao walimpa Yesu zawadi nyingi za dhahabu na marashi.
17


Mlungu aliwaonya Wenye Hekima wabwele ukae kwa siri. Herode kofura sana. Aliamua kumuangamiza Yesu, mtawala yule mwovu aliua wana wosi wa kiume huko Bethlehemu.
18


Lakini Herode hakuweza kumdhuru Mwana wa Mlungu! Alionywa katika ndoto, Yusufu alichukua Mariamu na Yesu kwa usalama huko Misri.
19


Herode alipokufa Yusufu alileta Mariamu na Yesu kutoka Misri.
Waliishi katika mji mdogo wa Nazareti, karibu na bahari ya Galilaya.
20

Kuzaliwa kwa Yesu

Hadithi ilawa kwa neon ja mlungu, Biblia,

hupatikana katika

Mathayo 1-2, Luka 1-2

"Kuingia kwa Maneno jako kolafa nuru."
Zaburi 119:130



# Mwisho

36 60



Hadithi ino ya Biblia yatulongela juu ya mlungu gwetu wa ajabu atuumbile kobama ummanye.

Mlungu komanya sosi titenda finu fikala fihile, ambayo koyakema zambi. Kolonga adhabu yake ni kifo, lakini mlungu kobama ng'ani akamlagiza mwana weeks. Yesu, afe msalabani na kumlaga dhambi shako. Kosha yesu kulamka na kubwela ukae mbinguni! Ikiwa unamwamini yesu na kumlomba akusamehe dhambi zako, kukwisa kukala mng'anda mwako sambi, na kukala nae milele.

Ikiwa unaamini ino ni kweli, longa fino komlungu "Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa gwegwe mlungu, na ukawa munu wa kufa kwa ajili ya dhambi zangu, na sambi kokala keli. Tafadhali iso maishani mwanguna ulongele dhambi zangu, ili niweze kuwa na maisha mapya sambi, na siku dimwe nigende nagwe milele. Nyafile kukutii na kukala kwa ajili yako kama mwanago. Amina".

Soma Biblia na longa na mlungu kila siku. Yohana 3:16